

TANGAZO LA KAZI – MADEREVA WA MALORI (NAFASI 07)



DCG
DSM CORRIDOR GROUP

MAELEZO YA NAFASI

DSM Corridor Group Ltd inatafuta kuajiri Madereva wa Malori katika Idara yake ya Ufundi (Technical Department). Waombaji watakaofanikiwa watahusika na uendeshaji wa malori makubwa na madogo kwa kuzingatia taratibu za kampuni pamoja na viwango vya usalama.

MAJUKUMU NA WAJIBU WA KAZI

1. Kusafirisha kwa usalama makontena na mizigo kati ya maeneo ya kampuni ya DCG, bandarini, na maeneo ya wateja kwa kuzingatia ratiba na njia zilizopangwa na kampuni.
2. Kufanya ukaguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kuhakikisha ubora wa gari, usafi, na uzingatiaji wa viwango vya usalama na matengenezo.
3. Kuhakikisha nyaraka za mizigo na usafirishaji zimekamili, ni sahihi, na zinafuata taratibu husika.
4. Kupakia na kushusha mizigo kwa kushirikiana na timu za ghala na bandarini huku ukihakikisha mizigo inalindwa dhidi ya uharibifu au upotevu.
5. Kuhakikisha mizigo inafikishwa kwa wakati na kuwasiliana na kitengo cha usafirishaji au msimamizi endapo kutatokea ucheleweshaji, ajali, au mabadiliko ya njia.
6. Kufuatilia matumizi ya mafuta na kutoa taarifa za kilomita, matumizi ya mafuta, na dosari zozote kwa msimamizi.
7. Kuwasilisha uthibitisho wa uwasilishaji wa mizigo (POD) pamoja na nyaraka husika mara baada ya safari kukamilika.
8. Kuzingatia kikamilifu sheria za barabarani, sera za usalama za kampuni, na maadili ya udereva wakati wote.
9. Kuripoti hitilafu au matatizo ya kiufundi kwa kitengo cha matengenezo mara moja.
10. Kushiriki katika ratiba za matengenezo ya magari ili kuhakikisha huduma za kinga zinafanyika kwa wakati.
11. Kutunza kumbukumbu za safari, taarifa za uwasilishaji, na taarifa sahihi za muda wa kazi.
12. Kufanya majukumu mengine yatakayopangwa na msimamizi, ikiwemo kuendesha vifaa vingine kama Forklift, Wheel Loader, Excavator, na Bobcat inapohitajika.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na Leseni halali ya udereva ya Tanzania – Daraja E na C.
2. Awe na uzoefu wa miaka 3–5 katika kuendesha malori makubwa au magari ya kubeba makontena kwenye sekta ya usafirishaji au mizigo.
3. Awe na uelewa wa shughuli za bandarini na taratibu za forodha.
4. Mafunzo ya udereva wa kujihami (Defensive Driving) au usalama barabarani yatakuwa faida ya ziada.
5. Awe na nidhamu, uwajibikaji, na uwezo mzuri wa kutunza muda.
6. Awe na cheti cha udereva kutoka taasisi inayotambulika.
7. Elimu ya angalau kidato cha nne inapendekezwa.
8. Awe na Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA.
9. Awe tayari kufanya kazi za zamu za usiku.
10. Awe mwaminifu, mwenye kujisimamia, na mwenye kuwajibika binafsi.
11. Uwezo wa kuendesha vifaa kama Forklift, Wheel Loader, Excavator, na Bobcat utakuwa faida.
12. Ujuzi wa matengenezo ya magari makubwa au vifaa vizito utaongeza nafasi ya kuajiriwa.



MALIPO

Kampuni itatoa mshahara na marupurupu ya ushindani kulingana na sheria za kazi. Mkataba wa kazi ni wa mwaka mmoja (1) na unaweza kuongezwa kulingana na utendaji wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA YA MAOMBI

Maombi yawasilishwe moja kwa moja katika dawati la mapokezi la Makao Makuu ya DSM Corridor Group, Plot No. 2A Bandari Road, Kurasini, au kupitia barua pepe: career@dsmcorridor.co.tz. Waombaji watakaofanikiwa wanaweza kuhitajika kupitia Ukaguzi wa kiusalama, tathmini ya uwezo wa kazi, ukaguzi wa afya ya mwili, Uhakiki wa taarifa za waombaji. Wanawake wanahimizwa sana kuomba nafasi hizi.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Tafadhali wasilisha maombi kabla ya tarehe 31/07/2026.